

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SITA

KIKAO CHA TANO

07 FEBRUARI, 2022



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SITA

KIKAO CHA TANO – TAREHE 07 FEBRUARI, 2022

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:

Maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.7) wa Mwaka 2021 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments)(No.7) Bill, 2021*].

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA:

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.7) wa Mwaka 2021 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.7) Bill, 2021*].

III. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

40. MHESHIMIWA DKT. THEA MEDARD NTARA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza ajira kwa Wahitimu wa Vyuo Vikuu hasa katika Sekta ya Kilimo.

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

41. MHESHIMIWA UHURU ALLY JUMA MAKOA (KONDOA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara muhimu ya Iboni – Bolisa – Gubalisa iliyopo katika Halmashauri ya Mji wa Kondoa kwa kiwango cha lami.

42. MHESHIMIWA ERIC JAMES SHIGONGO (BUCHOSA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itarejesha Mamlaka kwa Madiwani ya kuzisimamia Halmashauri zao pamoja na kuwaazimia Wakurugenzi wa Halmashauri pale linapotokea tatizo kwenye Halmashauri husika.

43. MHESHIMIWA SAMWEL XADAY HHAYUMA (HANANG’):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha Makao Makuu ya Tarafa za Basotu, Endasak na Balangdalah kunajengwa Vituo vya Afya.

WIZARA YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:

44. MHESHIMIWA NG'WASI DAMAS KAMANI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara:-

Je, Serikali imefikia hatua gani katika kuunganisha Mifuko ya Uwezeshaji Wananchi hususan Vijana na kuwa na eneo moja la wazi la utoaji huduma.

WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

45. MHESHIMIWA JOSEPHAT SINKAMBA KANDEGE (KALAMBO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-


Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya kuanzia Matai kwenda Kasesya *border* inayounganisha nchi yetu na Zambia.

46. MHESHIMIWA ANASTAZIA JAMES WAMBURA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itajenga *Air Traffic Control Tower* na jengo la muda la Abiria kwa ukubwa wa kutosha pamoja na *Parking shade* ya Mitambo ya Zimamoto na Uokoaji katika Uwanja wa Ndege wa Mtwara.

WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:



47. MHESHIMIWA NOAH LEMBURIS SAPUTU (ARUMERU MAGHARIBI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:-

Je, ni lini Serikali itayachukua Mashamba Pori yasiyoendelezwa kwa shughuli iliyokusudiwa yakiwepo mashamba ya Aghakan, Lucy *Estate* na Gomba *Estate* na kuyagawa kwa Wananchi.

WIZARA YA KILIMO:

**48. MHESHIMIWA JACKSON GEDION KISWAGA
(KALENGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, ni kwa nini Serikali isiwalipe angalau robo ya madai Mawakala wa mbolea za ruzuku katika Jimbo la Kalenga.

WIZARA YA MADINI:

**49. MHESHIMIWA SOPHIA HEBRON
MWAKAGENDA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Madini:-

Je, ni lini Mgodi wa Makaa ya mawe Kiwira utapata Mwekezaji mpya na kulipa mafao ya waliokuwa Wafanyakazi wa mgodi huo.

WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:

**50. MHESHIMIWA YUSTINA ARCADIUS RAHHI
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuchimba Malambo kwa ajili ya maji ya mifugo katika maeneo ya Wafugaji Mkoani Manyara.

WIZARA YA MAJI:

51. MHESHIMIWA ROBERT CHACHA MABOTO (BUNDA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

- Je, ni lini Serikali itasambaza maji katika Mitaa ya pembezoni kwa Kata za Kabasa, Guta, Kuzungu, Sazira, Nyatwali, Mcharo na Wariku katika Mji wa Bunda.

52. MHESHIMIWA JONAS WILLIAM MBUNDA (MBINGA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini Serikali itafikisha maji safi na salama katika Kata za Kilolo, Utiri, Mbangamao, Kilimani na Mateka.

WIZARA YA NISHATI:

53. MHESHIMIWA FESTO RICHARD SANGA (MAKETE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutekeleza Mradi wa REA katika Wilaya ya Makete ili kuhakikisha umeme unafika kila Kijiji.

IV. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

***[Kusomwa Mara ya Pili, Kamati ya Bunge Zima
na Kusomwa Mara ya Tatu]***

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.7) wa Mwaka 2021 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.7) Bill, 2021]*.

**DODOMA
07 FEBRUARI, 2022**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE**